**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**

Shule ya Sekondari Kishapu,
S.L.P 1240,
**SHINYANGA.**

**Simu Na. +255 752663188**
**+255 785764346**

15/12/2024

Kumb. Na.: KSS/JN/VOL I/2025/01
**Jina la Mwanafunzi: …………………………………**
**S.L.P ………………………………………………..**
**…………………………………………………………**

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISHAPU WILAYA YA KISHAPU MKOA WA SHINYANGA MWAKA 2025</u>**

## 1. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2025. Shule ya Sekondari Kishapu ipo umbali takribani kilometa 1.2 kutoka stendi kuu ya mji wa Mhunze.
Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **13/01/2025**, unatakiwa kuripoti shuleni ukiwa na **Mzazi/ Mlezi** kuanzia Tarehe **13/01/2025** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **30/01/2025**. ***(Mwanafunzi atakayeripoti bila*** **Mzazi/ Mlezi** ***wake hatapokelewa)***

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A. Sare ya Shule

#### (i) Wavulana

(a) Suruali mbili (2) rangi ya damu ya mzee, Suruali hizo ziwe na malinda mawili tu kama picha inavyoonesha chini, iwe na sm 16. Na si pungufu vinginevyo hatutampokea.

SEQ Figure * ARABIC 1 Mfano wa Suruali kwa wavulana

(b) Mashati mawili meupe mikono mifupi.
(c) T- Shirt itapatikana shuleni kwa Tshs. 12,000/= tu.

(d) Viatu vya Ngozi vyeusi vilivyo na Gidamu na kisigino (Jozi mbili).
(e) Soksi nyeusi ndefu (Jozi mbili)
(f) Tai ndefu ya Rangi ya damu ya mzee (Jozi mbili)
(g) Vifaa vya michezo kama vile Traki suti ya bluu bahari, raba/ viatu vya mpira.
(h) Sweta rangi ya damu yam zee,inapatikana shuleni kwa Tsh.15,000/=

**(ii) Wasichana**

(a) Sketi mbili (2) za rangi ya damu ya mzee, ndefu zinazozidi magoti. (Angalia mfano katika picha hapa chini).

SEQ Figure * ARABIC 2 Mfano wa Sketi kwa wasichana

(b) Mashati mawili meupe mikono mifupi.
(c) T- Shirt itapatikana shuleni kwa Tshs. 12,000/= tu.
(d) Viatu vya Ngozi vyeusi vilivyo na Gidamu na kisigino (Jozi mbili).
(e) Soksi nyeupe ndefu (Jozi mbili)
(f) Tai ndefu ya Rangi ya damu ya mzee (Jozi mbili)
(g) Vifaa vya michezo kama vile, Traki suti ya bluu bahari, raba/ viatu vya mpira.
(h) Sweta rangi ya damu yam zee,inapatikana shuleni kwa Tsh.15,000/

**B. VIFAA VYA DARASANI**

(i) Daftari (Counter Book) za kutosha masomo kumi na mbili (12)
(ii) Kalamu za kuandikia (pen) ya bluu au nyeusi, penseli na ufutio.
(iii) Mkebe mmoja (Mathematical set) pamoja na Rula ndefu (sm 30)
(iv) Bunda la karatasi (Ream A4) Moja kwa ajili ya majaribio na mitihani.

**C.VIFAA VYA USAFI**

( i) Chelewa 1

( ii)Ndoo ndogo 1

**MUHIMU; MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NA MFAGIO WA NJE (CHELEWA) KWA AJILI YA USAFI WA MAZINGIRA YA SHULE, MFAGIO HUO AUKABIDHI SIKU ANARIPOTI SHULE.**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na **Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi** yenye dhamana ya Elimu nchini na **Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) **Heshima** kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughulindani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini Maandalio ya jioni (Preparation) kwa wanafunzi wa Bweni.
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
(h) Kutunza mali za umma.

**Makosa Yanayoweza Kusababisha Kufukuzwa na Kusimamishwa Shule**

(a) Wizi.
(b) Uasherati, Ulawiti, Usagaji na Ushoga.
(c) Ubakaji.
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji **Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli**, na kadhalika.
(e) Kupiga au Kupigana
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa Mjamzito au Kupata Mimba.
(i) Kutoa Mimba.
(j) Kuoa au Kuolewa.

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kuwa na **SIMU** ya mkononi, **CAMERA, REDIO** na vitu vingine vyote vya kufanana na hivyo.

**KUKIRI**

Kama unakubali kujiunga na shule ya sekondari ya Isoso, Tafadhali jaza fomu zilizoambatanishwa na maelekezo/ Maagizo haya na uje nazo shuleni unaporipoti kwa mara ya kwanza.

**HITIMISHO**

Napenda tena kutumia fursa hii kukupongeza kwa kupata nafasi hii adimu ya kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza hapa Shule ya Sekondari Kishapu. Ni matumaini yangu hautaiacha nafasi hii Muhimu kwako ipotee bure.

**Hongera sana na Karibu Shule ya Sekondari Kishapu.**

**BUHORO NG'WANDU MIPAWA**

**MKUU WA SHULE**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**

---

**Anuani ya Mzazi/ Mlezi**
**……………………………………………….**
**……………………………………………….**
**……………………………………………….**
Tarehe**: ……………………..**

**Kumb. Na. KSS/JN/VOL 1/2021/02**
SHULE YA SEKONDARI KISHAPU
S.L.P 1240
**SHINYANGA.**

**YAH: <u>KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISHAPU</u>**

**A. MWANAFUNZI**

Mimi (Jina la Mwanafunzi) ……………………………............. (Herufi Kubwa), nimepokea, nimesoma na nimeelewa vizuri Masharti/ maelekezo ya kujiunga na masomo ya Sekondari Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Kishapu mwaka 2025. Na ninakubali kujiunga na Jumuiya ya Shule ya Sekondari Isoso, ninaahidi kutoshiriki katika Migomo, Fujo na Makosa ya jinai, nitakuwa mtiifu nitazingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za shule kama nitakavyoelekezwa.

***Sahihi ya Mwanafunzi***: …………………………………… ***Tarehe***: …………………………..

**B. MZAZI/ MLEZI**

**KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE**

MIMI (Jina la Mzazi/ Mlezi) ……………………………………… Mzazi/ Mlezi (Kata Isiyofaa) wa Mwanafunzi (Jina la mwanafunzi) …………………………………….. ninakiri kusoma na kuelewa Sheria, taratibu na kanuni pamoja na maelekezo ya shule. Ninaahidi kwa mujibu wa sheria na masharti yaliyoainishwa, nitashirikiana na kukubaliana na maelezo yote yatakayotolewa na Shule.

Kijiji ninachotoka ……………………………………… Kata ya …………………………………

Tarafa ya …………………………………….. Wilaya ya ………………………………………

Namba ya Simu (Mzazi/ Mlezi): ……………………………………………………

Sahihi (Mzazi/ Mlezi): …………………………….. Tarehe: ………………………………….

*(Karatasi hii Lazima irudishwe Shuleni ikiwa imejazwa)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

**A. MWANAFUNZI**

(i) Jina la Kwanza: …………………………………………………………………...
(ii) Jina la Kati: ……………………………………..........................................
(iii) Jina la Ukoo: …………………………………………………………………...

(**Majina haya lazima yabaki hivihivi kwa miaka yote uwapo shuleni Vinginevyo ulete Kiapo cha mahakama kinachoonesha umebadili jina)**

(iv) Tarehe ya Kuzaliwa: ……………………………………………………………….
(v) Mahali ulipozaliwa:
Wilaya: …………………………… Mkoa: …………………………………….
(vi) Dini: ……………………………… Dhehebu: ……………………………….
(vii) Shule uliyomaliza Darasa la Saba (VII): …………………………………………...

**B. BABA**

(i) Jina la Baba yako: …………………………………………………………………..
(ii) Yu hai? NDIYO/ HAPANA: ………………………………………………….
(iii) Kama amefariki taja tarehe: …………………………………………………...
(iv) Anuani yake: …………………………………………………………………..
(v) Namba ya Simu: ………………………………………………………………….
(vi) Kazi/ Cheo chake: …………………………………………………………………..
(vii) Dini ya Baba yako: ……………………... Dhehebu: ………………………………

**C. MAMA**

(i) Jina la Mama yako: …………………………………………………………………..
(ii) Yu hai? NDIYO/ HAPANA: ………………………………………………….
(iii) Kama amefariki taja tarehe: …………………………………………………...
(iv) Anuani yake: …………………………………………………………………..
(v) Namba ya Simu: ………………………………………………………………….
(vi) Kazi/ Cheo chake: …………………………………………………………………..
(vii) Dini ya Mama yako: ……………………... Dhehebu: ……………………………..

**D. MLEZI**

Mlezi ni mtu asiye Mzazi wako anayekutunza na kukuhudumia kwa chakula, malazi na mavazi.

(i) Jina la Mlezi wako: …………………………………….Jinsia (Me/Ke): …………
(ii) Uhusiano wako na Mlezi ni (Mjomba/Kaka/Rafiki/Shangazi/ n.k): ………………….
(iii) Anuani ya Mlezi wako: ………………………………………………………………
(iv) Kazi ya Mlezi wako: …………………………………………………………………
(v) Anaishi kitongoji gani? ……………………… Kata ya …………………………….
(vi) Jina la Mwenyekiti wa Kitongoji: …………………………… Simu: ………………

**E. KUKIRI (MWANAFUNZI)**

Ninakiri kuwa maelezo yote yaliyoandikwa hapo juu ni sahihi na ni ya ukweli.

Sahihi: ………………………………………….. Tarehe: ………………………………..

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## KISHAPU SECONDARY SCHOOL
## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**DATE: ………………….**

**PART A.**

Mr/ Miss ……………………………………………………………….

Please, Examine the above named person, his/ her Physical and Mental fitness for a full time learning. The examination should include the following categories: -

1. Eye
   Hearing
   Limbs
   Speech
   General Disease
   Leprosy
   Epilepsy

2. Neuroses
3. Other serious diseases
4. Pregnancy

**PART B.**

(To be completed by Government Medical Officer) I have examined the above-named person and consider that HIS/ HER is Physically *Fit/ Unfit and Mentally *Fit/ Unfit for full time learning.

1. Eye ……………………………………………………
   Hearing ……………………………………………………
   Limbs ……………………………………………………
   Speech ……………………………………………………
   General Disease ……………………………………………………
   Leprosy ……………………………………………………
   Epilepsy ……………………………………………………

2. Neuroses ……………………………………………………
3. Other serious diseases ……………………………………………………
4. Pregnancy …………………………………………………….

SIGNATURE: …………………………Stamp: …………………… DATE: …………………